**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

# UTARATIBU WA USAJILI WA VYAMA VYA SIASA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Kuundwa kwa chama cha siasa

Nchini Tanzania Chama cha Siasa kinaweza kuundwa kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Vyama vya Siasa kwa ajili ya kuendeleza malengo na madhumuni ambayo hayako kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar au sheria nyingine yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Kifungu cha 6(1)) cha Sheria ya Vyama vya Siasa.

### 1.2 Masharti ya kuanzisha chama cha siasa

Ukitaka kuanzisha chama cha siasa lazima ukubali masharti kwamba:-

(i) Vyama vya Siasa vilivyokuwapo Tanzania kabla ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar au kabla ya tarehe 05 Februari, 1977 haviwezi kusajiliwa tena. Vilevile jina au kifupi cha jina la vyama hivyo, hakiwezi kutumiwa na chama cha siasa chochote kilichosajiliwa Tanzania. (Kifungu cha 12(1)).

(ii) Chama hicho kitaendeshwa kwa kufuata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Katiba ya Zanzibar ya 1984, Sheria ya Vyama

vya Siasa Sura ya 258, katiba na Kanuni za chama husika, misingi ya demokrasia na utawala bora, kutokubagua, jinsi na ujumuishaji wa kijamii; na

(iii) Chama hicho kitadumisha Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mapinduzi ya Zanzibar, demokrasia, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa, maadili ya taifa, uzalendo, suala la Serikali kutofungamana na dini yoyote, mwenge wa uhuru, amani na utulivu wa taifa, masuala ya jinsia, vijana na ujumuishaji wa makundi maalum katika kijamii katika-

(a) uundaji na utekelezaji wa sera zake;
(b) uteuzi wa wagombea kwa ajili ya chaguzi; na
(c) uchaguzi wa viongozi wake.

**1.3 Usajili wa vyama vya siasa**

Usajili wa Vyama vya Siasa unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya Mwaka 1992 Sura ya 258 (The Political Parties Act CAP 258 RE: 2019) na Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa (The Political Parties (Registration and Monitoring) Regulations, 2019 GN 953).

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 7 cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kila chama cha siasa kilichoundwa katika upande wowote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kinapaswa kuomba kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa namna ilivyoelezwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa, kusajiliwa kama chama cha siasa (Kifungu cha 7(1)).

Sheria ya Vyama vya Siasa inasema kuwa, hakuna taasisi ambayo itafanya kazi kama chama cha siasa bila ya kusajiliwa kuwa chama cha siasa kwa mujibu wa Sheria hiyo (Kifungu cha 7(3)) cha Sheria ya vyama vya siasa

Kila chama cha siasa kitaanza kusajiliwa kwa muda na kupewa cheti cha usajili wa muda baada ya kutimiza masharti yaliyoainishwa katika kifungu cha 9 cha Sheria ya vyama vya siasa .

Kila chama cha siasa ambacho kilikuwa na usajili wa muda na ambacho pamoja na masharti ya kifungu cha 9 cha sheria hiyo, kimetimiza masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 10, kitatakiwa katika siku zisizozidi mia moja na themanini

kuanzia tarehe ya usajili wa muda kuwasilisha maombi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa ajili ya usajili kamili.

Usajili wa muda wa kila chama ambacho hakijawasilisha maombi ya usajili kamili utakoma na kila cheti cha usajili wa muda kitakoma kutumika baada ya kutimia kwa siku mia moja na themanini kutoka tarehe ya usajili huo wa muda.

Usajili wa muda wa chama ambacho kimeomba usajili kamili utakuwa halali hadi chama hicho kitakapopatiwa cheti cha usajili kamili au hadi maombi yake ya usajili kamili yatakapokataliwa.

Endapo katika maombi ya usajili wa chama cha siasa, ni wazi kwamba jina linalopendekezwa la chama cha siasa, kifupi cha jina lake au nembo ya chama-

(i) ni ya kutusi au kuchukiza;
(ii) inatumika na chama kingine cha siasa; au
(iii) imekuwa ikitumika na chama cha siasa ambacho cheti chake cha usajili kimefutwa au cheti cha usajili wa muda kimeisha muda wake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Msajili wa vyama vya siasa ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya kupokea maombi hayo atayakataa na kuwaarifu waombaji ipasavyo. (kifungu cha 8(6)(a-c) cha sheria ya vyama vya siasa).

Mtu anayewasilisha maombi ya usajili wa chama cha siasa lazima awe na sifa zifuatazo:-

(i) mtu huyo ni raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzaliwa na wazazi wake wote ni raia wa Jamhuri ya Muungano;
(ii) mtu huyo awe na akili timamu;
(iii) mtu huyo hajawahi kutangazwa na mahakama yenye mamlaka kamili kuwa amefilisika.
(iv) mtu huyo ametimiza umri wa miaka kumi na minane au zaidi;
(v) mtu huyo anaweza kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza; na
(vi) mtu huyo ndani ya miaka mitano kabla ya tarehe ya kuwasilisha maombi yake hajawahi kutiwa hatiani au kuhukumiwa kwa kutenda kosa la kukosa uaminifu, uhujumu uchumi, rushwa, ukwepaji kulipa

kodi au makosa yanayohusiana na ukatili wa kijinsia. (Kifungu cha 6B) cha Sheria ya vyama vya siasa

Msajili baada kuhakiki usahihi wa maombi ya usajili wa chama cha siasa na kuchambua maudhui ya maombi hayo, anaweza kukataa kusajili chama cha siasa, endapo kimeshindwa kutimiza matakwa na masharti ya usajili wa muda au kamili. Pale ambapo Msajili atakataa kusajili chama cha siasa, atatoa notisi ya maandishi kuhusiana na uamuzi wake akieleza sababu za kukataa kusajili. (Kanuni ya 10).ya Kanuni za usajili na ufuatiliaji

## 2.0 MAOMBI YA USAJILI WA MUDA

### 2.1 Nyaraka za kuwasilisha wakati wa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa maombi ya usajili wa muda

Watu waanaoomba usajili wa muda wa chama cha siasa watawasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nakala mbili ya fomu PP. 1 iliyojazwa kikamilifu. Fomu hiyo ipo katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za usajili na ufuatiliaji Maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo: –

(i) Tamko la kuthibitisha maombi katika Fomu PP.2 kama ilivyo kwenye Jedwali la Kwanza likiwa limejazwa kwa ukamilifu na kusainiwa na wanachama waanzilishi wawili wanaowasilisha maombi;
(ii) Nakala mbili za katiba na kanuni za chama zilizosainiwa na wanachama waanzilishi wawili wanaowasilisha maombi na zikiwa zimegongwa muhuri rasmi wa chama;
(iii) Nakala laini ya katiba na kanuni za chama;
(iv) Tamko la sera ya chama likijumuisha itikadi ya chama;
(v) Wasifu wa waanzilishi wawili wanaoomba usajili wa chama;
(vi) Cheti cha kuzaliwa na ushahidi wa uraia wa wanachama waanzilishi wawili wanaoomba usajili wa chama;
(vii) Uthibitisho wa uraia wa wazazi wa waanzilishi wawili wanaoomba usajili wa chama;
(viii) Picha mbili ndogo za kila mwanachama mwanzilishi anayewasilisha maombi ya usajili wa chama;
(ix) Mfano wa bendera ya chama katika kipande cha karatasi na nguo vyote vikiwa katika ukubwa wa A4;

(x) Mfano wa kadi ya uanachama; na

(xi) Uthibitisho wa malipo ya ada ya usajili wa muda ambayo ni Milioni Moja (Tshs. 1,000,000/=) (Kanuni ya 3(1)) ya kanuni za usajili na ufuatiliaji

Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Msajili anaweza kuhitaji taarifa za ziada zinazohusu matakwa na masharti ya usajili kama yalivyoainishwa katika Kanuni hizi na Sheria. (Kanuni ya 3(4)).

Kadi ya uanachama itajumuisha taarifa zifuatazo -

(i) jina la chama;

(ii) nembo ya chama;

(iii) namba ya kadi;

(iv) jina kamili la mwanachama;

(v) picha ndogo ya mwanachama;

(vi) saini ya mwanachama;

(vii) saini ya mamlaka inayotoa kitambulisho;

(viii) sehemu na tarehe kilipotolewa;

(ix) anwani ya posta na anwani ya makazi ya makao makuu ya chama; na

(x) taarifa yoyote ya ziada kama itakavyoidhinishwa na Msajili (Kanuni ya 3(3)).ya Kanuni za usajili na ufuatiliaji

Baada ya kupokea maombi ya usajili wa muda, Msajili atafanya yafuatayo:-

(i) Atatoa tangazo angalau kwenye magazeti mawili ambayo yanafika nchi nzima, moja likiwa la Kiswahili na lingine la Kiingereza, akikaribisha pingamizi kutoka kwa mtu yeyote au chama kingine chochote kuhusu jina alama au rangi ya chama kinachoomba usajili wa muda au suala lingine lolote linalohusu usajili wa chama cha siasa husika;

(ii) Atachambua nyaraka zilizoambatana na maombi ya usajili wa muda na anaweza kuelekeza zifanyiwe masahihisho au marekebisho ya nyaraka hizo.

(iii) Atawapa waliowasilisha maombi cheti cha usajili wa muda wa chama chao baada ya kuridhika kwamba, maombi ya usajili wa muda yamekidhi matakwa na masharti ya usajili.

## 2.2 Masharti ya Usajili wa Muda

Ili chama cha siasa kipate usajili wa muda kinapaswa kutimiza masharti yafuatayo:

Chama cha siasa hakitokuwa na sifa ya kupata usajili wa muda isipokuwa kama-

(a) wanachama waanzilishi wameomba usajili huo kwa namna ilivyoainishwa;
(b) maombi hayo yameambatana na nakala ya katiba ya chama cha siasa kilichopendekezwa;
(c) uanachama wake ni wa hiari na uko wazi kwa raia wote wa Jamhuri ya Muungano bila ubaguzi wa jinsia, ulemavu, imani ya dini, mbari, kabila, asili ya kabila, taaluma au kazi;
(d) uchaguzi wa viongozi wake katika Uchaguzi Mkuu uko wazi kwa jinsia zote (Kifungu cha 9(1)) cha sheria ya vyama vya siasa

Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), hakuna chama cha siasa kitachokuwa na sifa ya kupata usajili wa muda ikiwa, kwa katiba, kanuni na sera yake au vitendo vyake-

(a) kinakusudia kuhamasisha au kupigania maslahi ya-
  (i) imani yoyote ya kidini au kikundi;
  (ii) kabila lolote, asili ya jamii au kundi la kimbari; au
  (iii) eneo maalum ndani ya sehemu yeyote ya Jamhuri ya Muungano;
(b) kinahamasisha kuvunja umoja unaounda Jamhuri ya Muungano;
(c) kinakubali au kinahamasisha matumizi ya nguvu au vurugu kama njia ya kufikia malengo ya kisiasa;
(d) kinahamasisha au kinakusudia kuendesha shughuli zake za kisiasa katika sehemu moja tu ya Jamhuri ya Muungano; au
(e) hakiruhusu uchaguzi wa vipindi na wa kidemokrasia wa uongozi wake;
(f) kinaruhusu viongozi na wanachama wake kutamka au kutumia lugha chafu, visasi, kashfa au maneno ya uchochozi ambayo yanaweza kusababisha au kushawishi uvunjifu wa amani (Kifungu cha 9(1)).

## 3.0 HAKI ZA CHAMA CHENYE USAJILI WA MUDA NA MASHARTI YA KUTUMIA HAKI HIZO

Chama cha Siasa chenye usajili wa muda hakina haki ya kuweka mgombea au kufanya kampeni kwa mgombea yoyote katika uchaguzi wa ubunge, Rais au Serikali za Mitaa. Isipokuwa, kitakuwa na haki ya kufanya mikutano ya hadhara katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano, kwa lengo la kujitangaza au kutafuta wanachama, baada ya kutoa taarifa kwa afisa wa Polisi kiongozi wa eneo husika. Vile vile, kitakuwa na haki ya kupata ulinzi na msaada wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kwa lengo la kuwezesha mkutano kufanyika kwa amani na utulivu. (Kifungu cha 11(1)) cha sheria ya vyama vya siasa

Aidha, haki ya kufanya mikutano ya hadhara inaratibiwa na Sheria kadhaa, zikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 na Sheria ya Kuweka Utulivu Nchini Sura ya 385. Kwa mujibu wa Sheria hizi, Jeshi la Polisi lina mamlaka ya kisheria kuzuia chama cha siasa kisifanye mkutano wa hadhara au maandamano kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

## 4.0 MAOMBI YA USAJILI KAMILI

### 4.1 Nyaraka za kuwasilisha wakati wa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa maombi ya usajili kamili

Watu wanaoomba usajili kamili wa chama cha siasa watawasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nakala mbili ya fomu PP. 4 iliyojazwa kikamilifu. Fomu hiyo ipo katika Jedwali la Kwanza la Sheria ya Vyama vya Siasa. Maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo:

(a) tamko la kuthibitisha maombi katika Fomu PP.5 iliyowekwa kwenye Jedwali la Kwanza iliyojazwa kwa ukamilifu na kusainiwa na wanachama waanzilishi wawili wanaowasilisha maombi;
(b) nakala ya cheti cha usajili wa muda;
(c) idadi ya wanachama wa chama katika kila mkoa katika Fomu PP.5 A ikiambatana na orodha ya wanachama hao kwa mikoa, ikionyesha jina, jinsi, mkoa na namba ya kadi ya chama ya kila mwanachama;

(d) maelezo ya viongozi wa kitaifa wa chama katika Fomu PP.5 B ambayo itajumuisha jina, jinsi, anwani, namba ya simu, cheo, tarehe ya uteuzi au kuchaguliwa na sehemu anapotoka iwapo ni Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar na iambatane na;
   (i) uthibitisho wa uraia;
   (ii) kadi ya uanachama;
   (iii) wasifu;
   (iv) picha ndogo;
   (v) uthibitisho wa malipo ya ada ya usajili kamili;
   (vi) maelezo mengine yoyote kama yatakavyohitajika na Msajili yatakayokuwa ya lazima kwa madhumuni ya usajili;

(e) maelezo ya kila mwanachama mwanzilishi katika PP. 5C ambayo yatajumuisha jinsi,imani ya dini, mbari, kabila, kundi la asili, taaluma na kazi;

(f) mahali ilipo ofisi kuu au ofisi ndogo ya chama, anwani ya posta ya kila ofisi kwa msingi kwamba, kama ofisi kuu iko Tanzania Bara ofisi ndogo itakuwa Tanzania Zanzibar au kinyume chake katika Fomu PP.5D ikiambatana na nakala iliyohakikiwa ya mkataba wa pango au sehemu ya jengo au uthibitisho wa umiliki wa ardhi ambapo ofisi ya chama ipo;

(g) Uthibitisho wa malipo ya ada ya usajili kamili ambayo ni Shilingi Milioni Tano (Tshs. 5,000,000/=) (Kanuni 6).

Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Msajili anaweza kuomba taarifa za ziada kuhusu matakwa na masharti ya usajili yaliyoanishwa katika Kanuni hizi na Sheria. (Kanuni ya 6(2)).

Baada ya kupokea maombi yaliyofanywa chini ya Kanuni, Msajili atachambua nyaraka zinazothibitisha maombi ya usajili kamili na anaweza kuelekeza masahihisho au marekebisho ya nyaraka hizo. (Kanuni ya 6(3)).

## 4.2 Masharti ya Usajili Kamili

Ili chama cha siasa kipate usajili kamili kinapaswa kutimiza masharti yafuatayo:

Chama cha siasa hakitokuwa na sifa ya kupata usajili kamili isipokuwa kama-

(a) kwanza kimepata usajili wa muda;

(b) kimepata wanachama wasiopungua mia mbili ambao wana sifa ya kuandikishwa kama wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge kutoka angalau nusu ya mikoa ya Jamhuri ya Muungano ambayo kati yake angalau mikoa miwili iko Tanzania Zanzibar, mkoa mmoja kutoka Unguja na mkoa mwingine kutoka Pemba;
(c) kimewasilisha kwa Msajili majina ya wanachama wake kwa ajili ya uhakiki;
(d) kimewasilisha kwa Msajili mahali ilipo ofisi yake ya makao makuu na ofisi ndogo ya makao makuu kwa msingi kuwa kama ofisi kuu iko Tanzania Bara ofisi ndogo itakuwa Zanzibar;
(e) kwa kutumia katiba yake kimepiga marufuku wanachama wake kuwa na uanachama pacha;
(f) kimewasilisha majina ya uongozi wa kitaifa wa chama na uongozi huo unatokana na wanachama wake kutoka sehemu zote mbili Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara; na
(g) kimewasilisha kwa Msajili mahali ilipo ofisi yake ya makao makuu ndani ya Jamhuri ya Muungano na anwani ya posta ambapo notisi na taarifa nyingine zinaweza kutumwa. (Kifungu cha 10).

### 4.3 Sifa za kiongozi wa kitaifa wa chama cha siasa

Mtu atakuwa na sifa ya kugombea katika uchaguzi au kuteuliwa kuwa kiongozi wa chama cha siasa ikiwa mtu huyo-

(a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano ambaye ametimiza au ana umri wa Zaidi ya miaka ishirini na mmoja na anaweza kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
(b) mwanachama wa chama cha siasa husika;
(c) mtu ambaye, ndani ya miaka mitano kabla ya tarehe ya kuwasilisha jina kwa ajili ya uchaguzi au uteuzi, hajawahi kupatikana na hatia au kuhukumiwa kwa kutenda kosa la kukosa uaminifu, rushwa au kukwepa kulipa kodi;
(d) mtu mwenye akili timamu;
(e) mtu huyo hajawahi kutangazwa na mahakama yenye mamlaka kamili kuwa amefilisika; na

(f) hana sifa ya kusimamia ofisi ya umma chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano au Katiba ya Zanzibar ya 1984 au sheria nyingine yoyote (Kifungu cha 10A) cha sheria ya Vyama vya siasa

## 5.0 HAKI ZA CHAMA CHENYE USAJILI KAMILI NA MASHARTI YA KUTUMIA HAKI HIZO

Chama cha Siasa chenye usajili kamili kina haki zifuatazo:

i. Haki ya kufanya mikutano ya hadhara katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kujitangaza au kutafuta wanachama, baada ya kutoa taarifa kwa afisa wa Polisi kiongozi wa eneo husika;

ii. Haki ya kupata ulinzi na msaada wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kwa lengo la kuwezesha mkutano wa hadhara kufanyika kwa amani na utulivu.(Kifungu cha 11(1)) cha sheria ya Vyama vya siasa

iii. Haki ya kukata rufaa kwa Waziri wa mambo ya ndani, dhidi ya pingamizi la Polisi la kufanyika mkutano wa hadhara. Aidha, uamuzi wa Waziri ni wa mwisho. (Kifungu 43(6) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi wa akiba, Sura ya 322);

iv. Haki ya kuweka mgombea au kufanya kampeni kwa mgombea yoyote katika uchaguzi wa ubunge, Rais au Serikali za Mitaa (Kifungu cha 3 na 11(1)) cha sheria ya Vyama vya siasa

v. Haki ya kushirikiana baada ya kukamilisha masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa (Kifungu 11A) cha sheria ya Vyama vya siasa ;

vi. Haki ya kumiliki, kutumia na kuweka bendera yake katika maeneo ambayo yameanishwa na Sheria (Kifungu cha 11C) cha sheria ya Vyama vya siasa

vii. Haki ya kupata ruzuku endapo kina mbunge au diwani wa kuchaguliwa na kimetimiza masharti ya kupata ruzuku, yaliyopo katika Sheria ya Vyama vya Siasa. Mfano, kuwa na akaunti ya Benki (Kifungu cha 15(2), hesabu zake kukaguliwa na CAG (Kifungu cha 14(1)(b)(i) na kutumia fedha za ruzuku kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa inavyoelekeza (Kifungu cha 18).

viii. Haki ya kujieleza kabla ya usajili kamili kufutwa (Kifungu cha 19(2)(a) na (b);

ix. Haki ya kutofutiwa usajili kamili ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kuelekea Uchaguzi Mkuu (Kifungu 19(3)) cha sheria ya Vyama vya siasa

x. Haki ya kuomba Mahakama Kuu ifanye marejeo ya uamuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu usajili au kufuta usajili wa chama. (Kifungu cha 20(1)) cha sheria ya Vyama vya siasa

xi. Haki ya kuwa na wawakilishi wawili katika Baraza la Vyama vya Siasa, ambao ni viongozi wa kitaifa (Kifungu cha 21B(2))

Aidha, haki ya kufanya mikutano ya hadhara inaratibiwa na Sheria kadhaa, zikiwamo, Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 na Sheria ya Kuweka Utulivu Nchini Sura ya 385. Kwa mujibu wa Sheria hizi, Jeshi la Polisi lina mamlaka ya kisheria kuzuia chama cha siasa kisifanye mkutano wa hadhara au maandamano, kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

## 6.0 KUFUTWA KWA USAJILI WA CHAMA CHA SIASA

Msajili wa Vyama vya Siasa anaweza kufuta usajili wa chama cha siasa, ambacho kimekiuka kifungu chochote cha Sheria ya Vyama vya Siasa au kimepoteza sifa za usajili. (Kifungu cha 19(1)).

Uamuzi wa Msajili wa kuhusu usajili na kufuta usajili wa chama cha siasa ni wa mwisho, na hauwezi katiwa rufaa mahakamani (Kifungu cha 20(1)), isipokuwa, kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu cha 20 cha sheria ya Vyama vya siasa, hakikatazi mtu kuomba Mahakama kufanya marejeo ya uamuzi wa Msajili.